HOTUBA YA MHE. PROF. PETER MSOLLA (MB) WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA WAKATI WA UZINDUZI WA BODI YA NNE YA WAKURUGENZI YA SHIRIKA LA POSTA TANZANIA, KATIKA HOTELI YA PROTEA (COURTYARD) DAR ES SALAAM

TAREHE 6 MACHI, 2009

- Dr. Naomi B. Katunzi, Katibu Mkuu, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia,
- Dr. Yamungu Kayandabila, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Posta Tanzania,
- Ndugu Wajumbe wa Bodi,
- Kaimu Postamasta Mkuu,
- Wageni Waalikwa,
- Wanahabari,
- Mabibi na Mabwana,

1. Awali ya yote napenda nichukue fursa hii kushukuru uongozi wa Shirika la Posta Tanzania kwa kunialika kuwa mgeni rasmi katika uzinduzi wa Bodi ya nne ya Wakurugenzi ya Shirika la Posta Tanzania. Aidha, ninampongeza Dr. Yamungu Kayandabila kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Mwenyekiti wa Bodi hii, ndugu Idrisa Kilangi kwa kuteuliwa na wajumbe wa Bodi kuwa Makamu wa Mwenyekiti. Ninawapongeza sana Wajumbe wote kwa kuteuliwa kwenu kwa niaba ya Wizara na kwa niaba yangu mwenyewe, ninapenda kuishukuru Menejimenti ya Shirika la Posta kwa kunipa heshima ya kuzindua Bodi hii mpya. Asanteni sana.

2. Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi,

Kama wote tunavyofahamu, kwa mujibu wa Sheria ya Bunge Na. 19 ya mwaka 1993 iliyoanzisha Shirika la Posta, Bodi ya Wakurugenzi inatakiwa kuwa na Mwenyekiti na wajumbe wasiopungua wanne lakini wasiozidi sita. Chini ya sheria hiyo, Mwenyekiti anateuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo wajumbe wanateuliwa na Waziri mwenye dhamana ya kusimamia Sekta ya Posta.

Hivyo kuteuliwa kwenu ni kielelezo tosha cha imani kubwa ambayo serikali inayo kwenu. Ninawapongeza sana kwa kuteuliwa kwenu na ninawatakia mafanikio katika utekelezaji wa majukumu yaliyopo mbele yetu. Aidha, napenda nichukue fursa hii pia kuishukuru Bodi iliyomaliza muda wake kwa utumishi mzuri wa kusimamia utendaji kazi katika Shirika hili kwa kipindi kilichopita.

Mchango wa Bodi iliyopita umeendeleza uhai wa Shirika letu na kulijengea sera na mipango endelevu. Nakuagiza Kaimu Postamasta Mkuu ufikishe shukrani zangu hizi kwa wajumbe wote wa Bodi waliomaliza muda wao.

3. Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi,

Historia na asili ya huduma za Posta inatokana na mahitaji yaliyojitokeza katika kurahisisha utawala wa himaya za mwanzo kama za Uchina, Roma, Misri na Uajemi ambako kulikuwa na mfumo wa watawala kuwasiliana

miongoni mwao kwa kutumia tarishi wanaotembea kwa miguu au kwa farasi ambao walikuwa wanapokezana taarifa za maandishi au za mdomo.

Enzi hizo za ustaarabu wa mwanzo wa binadamu, watawala pekee ndio walikuwa wana haki ya kutumia mfumo huo pekee wa mawasiliano. Lakini, kutokana na umuhimu na kasi ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya binadamu, mfumo wa utoaji wa huduma za mawasiliano uliendelea kuboreshwa ambapo hadi kufikia karne ya 16 ilianza kuwa ya kisasa zaidi.

Kwa hivi sasa huduma za Posta ndizo zenye mtandao mkubwa zaidi duniani na zinatumiwa na kuwafikia watu wengi zaidi ikilinganishwa na zama zile za kale ambapo zilikuwa ni huduma maalum kwa ajili ya watawala tu.

4. Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi,

Kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Umoja wa Posta Duniani (UPU) mtandao wa mawasiliano kwa njia ya Posta unajumuisha ofisi za posta laki sita na sitini elfu (660,000) na wafanyakazi wapatao milioni nne na nusu (4.5 milioni) wenye ajira za kudumu na takribani milioni moja wenye ajira za muda (part-time employees). Huu ni mtandao mkubwa zaidi duniani ukiwa na uwezo wa kusambaza wastani wa barua zipatazo 439.0 bilioni na vifurushi 6.2 bilioni kwa mwaka.

Kwa upande wa bara la Afrika, kuna posta kamili 15,799 zinazoendeshwa na wafanyakazi wenye ajira ya kudumu ambazo ni wastani wa asilimia 2.3 ya ofisi za posta zilizopo ulimwenguni ambapo asilimia 13 ya watu wote duniani wanaishi katika bara la Afrika. Licha ya kwamba hapa Barani Afrika mtandao wa huduma za posta ni mpana zaidi ikilinganishwa na hapo awali, wastani wa watu wanaohudumiwa na ofisi moja ya posta ni zaidi ya 82,000 ikilinganishwa na kiwango kinachokubalika kimataifa cha wastani wa watu 5,000.

Aidha ni asilimia 23 tu ya wakazi wa bara la Afrika wanaofikishiwa barua, nyaraka, vifurushi na vipeto katika makazi yao (physical delivery of mail) ikilinganishwa na 83% Latini Amerika, 94% bara la Asia na 98% nchi zilizoendelea (industrialized countries).

Kwa upande wa Tanzania, wastani wa watu 80,000 wanahudumiwa na ofisi moja ya posta. Kuhusu ufikishaji barua na vifurushi katika makazi ya watu (physical delivery of mail) kiwango ni kidogo sana. Wastani wa asilimia 98 ya barua hupitia katika masanduku ya barua yaliyoko katika ofisi za posta.

Kiwango hiki kinaonyesha wazi kuwa tunalo jukumu la msingi la kupanua na kuboresha mtandao wa huduma za posta hapa nchini ili kufikisha huduma hizo karibu zaidi na jamii.

5. Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi,

Ningependa kuchukua fursa hii kuwakumbusha juu ya majukumu makuu ya Shirika hili kama yalivyoainishwa kwenye sehemu ya Tatu ya Sheria iliyoanzisha Shirika hili. Majukumu hayo ni pamoja na:-

- Kutoa huduma za Posta ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

- Kuweka mipango ya kuhakikisha huduma za msingi za Posta zinasambazwa nchini kote ili kukidhi mahitaji ya msingi ya mawasiliano kwa jamii (Public Service Obligation);
- Kutoa huduma za utumaji na ulipaji wa hati za fedha, hundi na hawala za Posta katika mtandao wa kaunta za Posta;
- Kutoa huduma za uwakala na huduma nyingine zinazohitajika kwa jamii kupitia mtandao wa Posta kwa lengo la kuliimarisha Shirika kibiashara; na
- Kutokana na umuhimu wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA), Shirika pia linao wajibu wa kuchochea na kusambaza matumizi ya teknolojia ya kisasa ili kuwarahisishia wananchi wa mijini na vijijini kujiletea maendeleo na uendeshaji wa maisha yao ya kila siku.
    * Kwa mujibu wa sheria hiyo, Shirika linaweza kuanzisha kampuni tanzu (subsidiary company) ambayo hisa zote au baadhi yake zinapangwa na kumilikiwa na Shirika.

6. Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi,

Sehemu ya pili ya Sheria ya Bunge iliyoanzisha Shirika hili pia imeainisha vizuri majukumu ya Bodi ambayo ni chombo cha juu kabisa cha utoaji wa maamuzi ndani ya Shirika hili. Kwa muhtasari majukumu hayo ni kama ifuatavyo:

- Kuidhinisha Bajeti ya mapato na matumizi ya kila mwaka ya Shirika.
- Kupitia na kuridhia mipango ya maendeleo ya Shirika.
- Kutoa maamuzi juu ya uwekezaji mitaji katika miradi ya Shirika. Kwa mfano, ipo changamoto kuhusu matumizi bora ya jengo la Posta ya Zamani pamoja na lile la Makao Makuu katika kuongeza mapato ya Shirika.
- Kuidhinisha kiwango kinachoweza kukopwa kutoka taasisi za fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Shirika.
- Kuidhinisha Sera mbalimbali zinazohusu utoaji wa huduma na uendeshaji.
- Kuidhinisha ikama ya Shirika na muundo wa utumishi pamoja na miundo ya mishahara na mafao mbalimbali yanayoendana na sera na masuala ya ajira ikiwa ni pamoja na pensheni za wafanyakazi wa Shirika.
- Bodi inawajibika vile vile na usimamizi wa upangaji wa ada/bei mbalimbali za huduma zinazotolewa na Shirika la Posta Tanzania kwa lengo la kuhakikisha kuwa shughuli za Shirika zinaendeshwa kwa misingi ya biashara na kupata faida.

7. Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi,

Eneo mojawapo ambalo Serikali inalisimamia na ambalo linagusa pia wadau wengine wa huduma za Posta ambao ni pamoja na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na makampuni binafsi yanayotoa huduma hizi (private operators), ni utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Sekta ya Posta ya Mwaka 2003 (National Postal Policy).

Mwelekeo wa Sera ya posta (National Postal Policy) kwa muhtasari ni:

- Kuwa na huduma za msingi za posta ambazo zinatolewa kwa ufanisi na zinaifikia jamii yote kwa gharama nafuu.
- Kuendeleza mazingira ya ushindani katika utoaji wa huduma za posta nchini.
- Kuzifanya huduma za posta kuwa za kisasa zaidi kwa kutumia teknolojia maridhawa ili kukidhi mahitaji mapya ya wateja ambayo yanabadilika mara kwa mara.
- Kuliendesha Shirika la Posta kwa misingi ya kibiashara, na
- Kushirikisha sekta binafsi katika kuendesha na kuwekeza katika shughuli na mtandao wa posta ili kuchochea maendeleo ya sekta hiyo.

Aidha, sera inasisitiza umuhimu wa kuendeleza rasilimali watu, kuimarisha usalama katika utoaji wa huduma za posta na kuanzisha mfumo mpya wa anuani za makazi (physical addressing and postcode system). Mradi huu ambao unasimamiwa na Mamlaka ya Kudhibiti Mawasiliano (TCRA) ni mtambuka na utarahisisha na kuboresha masuala ya kiuchumi na kijamii.

8. Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi,

Serikali ndiyo mmiliki wa Shirika la Posta kwa asilimia 100. Kwa kipindi kirefu sasa Shirika limekabiliwa na madeni na limeshindwa kuimarisha mtaji wake wa biashara (working capital) na hivyo kukosa nguvu ya kifedha ya kupanua na kuboresha mtandao wake pamoja na vitendea kazi.

Kutokana na hali hiyo, Serikali ya awamu ya nne inayoongozwa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetoa maamuzi muhimu yenye lengo la kupunguza matatizo hayo ikiwa ni pamoja na uamuzi wa kufuta na kuchukua madeni ambayo yamedumu kwa kipindi kirefu, mengi yakiwa yamerithiwa kutoka Shirika la zamani la Posta na Simu Tanzania (TP&TC).

Aidha, Serikali imerejesha jengo la Posta la zamani lililoko mtaa wa Sokoine na Mkwepu, Dar es Salaam chini ya miliki ya Shirika la Posta ili jengo hilo litumike kama kitega uchumi, hivyo kuongeza mapato ya Shirika.

9. Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi,

Baada ya kuwaeleza kuhusu sera ya Taifa ya Sekta ya Posta, sheria ya Bunge iliyoanzisha Shirika la Posta, majukumu ya Shirika na yale ya Bodi na kwa kutambua kwamba:

- Serikali imechukua na kufuta madeni ya Posta,
- Jengo la Posta la zamani limerudishwa mikononi mwa Posta,
- Jengo la sasa la Posta kutokutumika kikamilifu,
- Kuwa na mtandao mkubwa wa Posta nchini, na
- Uwezekano mkubwa wa Shirika kukopesheka;

Nachukua nafasi hii kutoa maelekezo ya Serikali ambayo yanapaswa kuzingatiwa na Bodi katika mchakato wa kulikwamua na kuliendeleza Shirika la Posta kama ifuatavyo:

(i) Kufuatilia kwa karibu mchakato wa kufuta na kuchukua madeni ya muda mrefu ili kusafisha mizania ya Shirika.

(ii) Kushirikiana kwa karibu na HAZINA katika mazungumzo na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ili wakabidhiwe jukumu la kulipa pensheni za wafanyakazi na wastaafu waliotokea Shirika la Posta na Simu la Afrika Mashariki.

(iii) Kubuni mipango na mikakati mbalimbali ya kuboresha mtaji wa Shirika.

(iv) Kufanya upembuzi yakinifu wa majengo na viwanja vinavyomilikiwa na Shirika na kuweka mipango endelevu na madhubuti ya kuendeleza kwa kutumia mikopo na kuingia mikataba na wabia ili kujenga majengo makubwa ya kisasa na ya kibiashara hivyo kuwa na chanzo muhimu cha mapato ya Shirika.

(v) Uongozi wa Shirika la Posta uwe wenye kuleta tija na kubana matumizi hususan kuboresha ofisi za mikoa na kuangalia upya kama upo umuhimu wa kuwepo ofisi za Kanda.

(vi) Kufanya mapitio ya mifumo ya uendeshaji na muundo wa Shirika ili kuisuka upya safu ya uongozi kwa lengo la kupunguza urasimu na uzembe, kuongeza ubunifu na unyumbufu (flexibility) na muhimu zaidi kuleta ufanisi katika kuliendesha Shirika kwa misingi ya kibiashara. Uongozi wa shirika utekeleze majukumu yake kuendana na wakati na wala siyo kwa kutumia mazoea.

(vii) Kuendeleza rasilimali watu hususan katika matumizi ya TEKNOHAMA na kuendesha shughuli za Posta kwa misingi ya kibiashara pamoja na kuongeza ujuzi na kuboresha mtizamo wao katika dhana ya huduma bora kwa wateja katika mazingira ya ushindani wa kibiashara.

(viii) Kila mwaka ifanyike tathmini ya kupima utendaji wa kazi wa kila mfanyakazi ili matokeo ya zoezi hilo yasaidie katika kuchukua hatua za marekebisho pale yatakapohitajika.

(ix) Kuwekeza katika matumizi ya teknolojia mpya na ya kisasa hususan TEKNOHAMA ili kuboresha huduma zilizopo kuanzisha huduma mpya zinazokwenda na wakati. Wizara yangu ingependa kuona ofisi zote za Posta zinatoa huduma za internet, hybrid mail, electronic money transfer na kulipa pensheni za wastaafu na mishahara ya watumishi wa Serikali na zile za sekta binafsi walioko vijijini.

Maelekezo haya yakitekelezwa kikamilifu pamoja na Menejimenti ya Shirika kujiimarisha katika kukabiliana na changamoto zilizopo na kutumia vizuri fursa mpya za kibiashara, ni dhahiri kuwa Shirika litaweza kusonga mbele, kuwa imara zaidi na kuchangia ipasavyo katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi hivyo, kubadilisha taswira yake mbele ya wadau na jamii kwa ujumla.

10. ***Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi,***

Penye nia pana njia. Yote niliyoyataja yanawezekana kufanyika, cha msingi ni Bodi hii, Menejimenti na wafanyakazi wote wa Posta waliosambaa nchi nzima, kufanya kazi kwa ufanisi na kwa mafanikio ya Shirika hili, ambayo pia ni mafanikio ya wadau na watanznia wote.

Jambo moja ambalo inabidi mlizingatie ni kwamba Watanzania wana matumaini na matarajio kuwa Shirika hili lichangie katika kuwaletea maendeleo yao. Wanawategemea ninyi, kuwa mtakuwa sehemu muhimu ya kuleta maboresho na mabadiliko wanayopenda kuyaona yakitolewa.

11. ***Ndugu Mwenyekiti,***

Kabla sijazindua Bodi hii mpya napenda niwakabidhi kila mjumbe wa Bodi kabrasha lenye nyaraka muhimu zinazohusu shirika letu la Posta ili ziwe nyenzo muhimu za kufanyia kazi.

12. ***Ndugu Mwenyekiti,***

Baada ya kuyasema haya napenda niwashukuru tena kwa kunikaribisha na kunipa fursa ya kuzungumza. **Sasa natamka kuwa Bodi ya Nne ya Wakurugenzi ya Shirika la Posta imezinduliwa rasmi.**

=AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA=